**MTIHANI WA KUTATHIMINI WILAYA YA BONDO - 2015**
**Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)**
102/1
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 1**
Julai/Agosti- 2015
**MUDA: SAA 1 ¾ Hours**
**MWONGOZO**

1. - Ni insha ya ripoti.
   - Mtahiniwa azingatie sura ya ripoti.
   - Asipozingatia sure hii,aondolewe alama 45 baada ya kusahihisha.

Chanzo cha mgomo
- Wanahitaji nyongeza ya mshahara.
- Ukosefu wa vifaa vya kufanyia kazi.
- Mazingira chafu.
- Kutokubaliwa na serikali kuunda chama chao cha kuwatetea.
- Uhaba wa dawa hospitalini.

<u>Suluhu</u>
- Waongezewe mshahara.
- Mishahara yao ilipwe kwa wakati ufaao.
- Vifaa vya kuufanyia kazi vinunuliwe.
- Wakubaliwe kuukdna chama chao.

n.k

Kadiria hoja za mtahiniwa.

2. Hii ni insha ya methali.
   Maana:
   - Mtu mwenye shida akieleza ,kusaidiwa bali asipoeleza hawezi kusaidiwa.

   Matumizi
   - Atesekaye kimya kimya bila ya kuomba msaada huzinduliwa kwa methali hii.
   - Mtahiniwa asimulie kisa kinachoonyesha alivyoteseka pasi na kusema mpaka alipoamua kusema ndipo akapata msaada.
   - Mtahiniwa ashughulikie pande zote mbili za methali.
3. Mtahiniwa arejelee vijana wa kiume,akirejelea vijana wa kike au wa kike na kiume,achukuliwe kuwa amejitungia swali.

Changamoto
- Ajira ya mapema.
- Ndoa za mapema.
- Ukosefu wa ajira.
- Kutopewa elimu ya kutosha.
- Dawa za kulevya.
- Uvunjaji wa sheria (kuingizwa kwa ujambazi)

n.k

Hatua
- Hatua kali ichukuliwe dhidi ya waajiri wa watoto.
- Waelimishwe kuhusu madhara ya ndoa za mapema.
- Serikali ibuni nafasi nyingi za kazi na kupendekezea vijana kujiajiri.
- Kuwe na elimu bila malipo.
- Kuelimishwa kuhusu madhara ya dawa za kulevya.

n.k

Kadiria hoja za mtahiniwa.

4. Hii ni insha ya mdokezo.
   - Mtahiniwa aanze kwa mdokezo aliopewa akibadilisha,atakuwa amejitungia swali.
   - Swali linakadiria uwezo wa mwanafunzi kubuni kisa kitakachoanzia kwa

mdokezo aliopewa.
- Maudhui yauone na maneno ya utangulizi.
- Masaibu ya kufutilia mbali kwa matokeao ya mtihani.
- Ataje yaliyofanya mtihani kufutiliwa mbali.
- Msisimko kwa wanafunzi.
- Hatua zilizochukuliwa.

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA INSHA TOLEO LA 2013**

**UTANGULIZI**

Karatasi hii imedhamiria kutathimini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi,akizingatia mada aliyopewa.Mawasilianno haya yanategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa.kwa mfano,kutunga sentensi zenye mtiririrko mzuri kimawazo asilia,ubunifu mwingi na hati nadhifu.Kwa kutegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha,ni lazima kutilia mkazo mtindo,mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo.Mtahini lazima aisome insha yote huku akizingatia sarufi,hijai,hoja,msamiati na mtindo ili aweze kuikadiria kwa kurejelea viwango mbalimbali vilivyopendekezwa.Viwango vyenyewe ni A,B,C na D kutegemea uwezo na mtahiniwa.

**VIWANGO MBALIMBALI**

**KIWANGO CHA D KWA JUMLA MAKI 01 – 05.**

1. Insha haieleweki kwa vyovyote vile ama uwezo wa mtahiniwa wa kutumia lugha nadhifu sana,hivi kwamba mtahini lazima afikirie kile mtahiniwa anachojaribu kuwasilisha.
2. mtahiniwa hana uwezo wa kutumia manene ya Kiswahili kwa njia inayofaa.
3. Lugha imevurugika ,uakifishaji haufai na insha ina makosa ya kila aina.
4. Kujitungia swali na kulijibu.
5. Insha ya urefu wa robo ikadiriwa hapa.

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA D**

**D- (D YA CHINI) MAKI 01-02**

1. Insha haina mpangilio maalum na haieleweki kwa vyovyote vile.
2. Kujitungia swali tofauti na kilijibu.
3. Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili au kuchanganya ndimi.
4. Kunakili swali au kichwa tu.

**D WASTANI MAKI 03**

1. Mtirirriko wa mawazo haupo.
2. Mtahiniwa amepotoka kimaudhui.
3. Matumizi ya lugha ni hafifu mno.
4. Kuna makosa mengi ya kila aina.

**D+(D YA JUU)MAKI 04 – 05)**

1. Insha ya aina hii huwa na makosa mengi ya kila aina.Lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kuwasilisha.
2. Hoja hazikuelezwa kimakinifu/mada haikukuzwa vilivyo.
3. Mtahiniwa hana uhakika wa matumizi ya lugha.
4. Mtahiniwa hujirudiarudia.
5. Insha itakayozingatia sura lakini ikose maudhui ikadiriwe hapa.

**KIWANGO CHA JUMLA MAKI 06 - 10**

1. Mtahiniwa anaj anajarubu kushughulikia mada japo hakuikuza na kukiendeleza vilivyo
2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe **kwa** njia isiyovutia/ hana ubinifu wa kutosha.sentensi vihaya.
3. Mtahiniwa anakifisha sentensi vibaya.
4. Mtiririrko wa rnawazo unaanza kujitokeza japo kwa njia hafifu.
5. Insha ina makosa mengi ya sarufi,ya msamiati ya tahajia.(hijai).

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA C**

**C – (C YA CHINI)MAKI 06 – 07**

1. Mtahiniwa anashida ya kuwasilisha na kutiririsha mawazo yake.

2. Mtahiniwa hana msamiati wa kutosha wala miundo ya sentensi ifaayo.
3. Mtahiniwa anafanya makosa mengi ya sarufi,ya hijai na msamiati na insha yake haieleweki kwa urahisi.

**C WASTANI MAKI 08**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu
2. Dhana tofautitofauti hazijitokezi wazi.
3. Mtahimvva hana ubunifu kutoshâ.
4. Mtiririko wa mawazo n**i** hafifu na hana ufundi *wa* lugha inayofaa.
5. Amejaribu kushughulikia mada aliyopewa.
6. Mtahiniwa ana shida ya uakifishaji.
7. Mtahiniwa anafanya makosa mengi ya **sarufi**, ya hij**ai na ya msamiati** lakini bado insha inaeleweka.

**C+(C YA JUU MAKI 09 – 10**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri akizingatia mada lakini kwa njia isiyo na mvuto.
2. Dhana tofauti tofauti zimejitokeza japo kwa njia hafifu.
3. Kuna mtiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa.
4. Misemo na methali zimetumika kwa njia hafifu.
5. Ana shida ya uakifishaji.
6. Kuna makosa ya sarufi,ya msamiati na hijai yanayoathiri mtiririko wa mawazo.

**KIWANGO CHA B KWA JUMLA MAKI 11 – 15**

1. Katika kiwango hiki,mtahiniwa anaonyesha hali ya kuimudu lugha.
2. Mtahiniwa anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri.
3. Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha.
4. Mada imekuzwa na kuendelezwa kikamilifu.
5. Insha ya urefu wa robo tatu ikadiriwe katika kiwango hiki.

**NGAZI MBAL1MBAL1 *ZA* KIWANGO CHA B**

**B -(B YA CHINI MAKI 11-12**

1. Mtahiniwaanawasilisha ujumbe ujumbe vizui kwa kueleza hola tofauti tofauti akizingatia mada.
2. Mtahiniwa ana mtiririko mzuri wa mawazo.
3. Mtahiniwa anatumia mifano michache ya msamiati unaovutia.
4. Makosa yanadhihirika /kiasi.

**B WASTANI MAKI 13**

1. Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kumudu lugha.
2. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika akizingatia mada.
3. Myahiniwa anateua na kutumia mifano michache ya msamiati mwafaka.
4. Sarufi yake ni nzuri.
5. Makosa ni machache /kuna makosa machache.

**B+ (B YA JUU) MAKI 14 – 15.**

1. Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika na anajieleza waziwazi.
2. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia inayovutia na kwa urahisi akizinatia mada.
3. Mtahiniwa ana mchanganyiko mzuri wa msamiati unaofaa.
4. Sarufi yake ni nzuri.
5. Uakifishaji wa sentensi zake ni mzuri.
6. Makosa ni machache ya hapa cia pale.

**KIWANGO CHA A KWA JUMLA MAKI 16-20**

1. Mtahiniwa ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka akizingatia mada.
2. Mtahiniwa anadhhihirisha ujuzi wa lugha yenye mnato.
3. Ana uwezo wa kutumia tamathali za usemi i1i kutoa hisia zake kwa njia bora

na kwa urahisi.
4. Umbuji wake unadhihirisha ukomavu na ukakamavu wake kimawazo.
5. Insha insaurefu kamili.

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA A**
**A- (A YA CHINI) MAKI 16 – 17**

1. Mtahiniwa anadhihirisha ukomavu wa lugha.
2. Mwazo ya mtahiniwa yanadhihirika na anashughulikia mada.
3. Ana mtirirko mzuri wa mawazo.
4. Msamiati wake ni mzuri na unaovutia.
5. Sarufi yake ni mzuri.
6. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
7. Makosa ni machache yasiyokusudiwa.

**A WASTANI MAKI 18**

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizur kilingana na mada.
2. Anajieleza kikanhilifu akitumia lugha ya mnato.
3. Anatoa hoja zilizokomaa.
4. Anatumia msamiati wa hali ya juu na unaovutia zaidi.
5. Anatumia miundo tofauti totafauti ya sentensi kiufundi**.**
6. Makosa ni nadra kupatikana.

**A+ (A YA JUU) MAKI 19 – 20.**

1. Mawazo yanadhihirika zaidi na mada imeshughulikiwa viiivyo.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lughaa ya mnato
3. Hoja zake zimekomaa na zinashawishi.
4. Msamiati wake ni wa hali ya juu na unaovutia zaidi.
5. Sarufi yake nzuri zaidi.
6. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
7. Makosa yote kwa jumla hayazidi <u>matano.</u>

**<u>VIWANGO MBALIMBALI KWA MUHTASARI</u>**

| KIWANGO | NGAZI | MAKI |
|---|---|---|
| A | A+<br>A<br>A- | 19 – 20<br>18<br>16 - 17 |
| B | B+<br>B<br>B- | 14 – 15<br>13<br>11 - 12 |
| C | C+<br>C<br>C- | 09 – 10<br>08<br>06 07 |

| | | |
|---|---|---|
| D | D+<br>D<br>D- | 04 – 05<br>03<br>01 - 02 |

b,Majina ya pekee

(i) Mjina ya mahali,mji,nchi,mataifa na kadhalika.
(ii) Siku za juma,miezi n.k.
(iii) Mshirika,masomo,vitabu n.k.
(iv) Makabila,lugha n.k.
(v) Jina la Mungu.
(vi) Majina ya kutambulisha hasa wanyama wa kufugwa,kwa mfano yale ya mbwa – Foksi,Ja,Popi,Simba,Tom na mengineyo.

## MAKOSA YA HIJAI/TAHAJIA

Haya ni makosa ya maendelezo. Mtahini anashauriwa asahihishe huku *akiyaonyesha* yanapotokea kwa mara ya kwanza tu. Makosa ya tahajia huweza kutokea katika:

(a) Kutenganisha neno kwa mfano 'aliye kuwa'
(b) Kuunganisha maneno kwa mfino 'kwasababu'.
(c) Kukata silabi visivyo afikapo pambizoni kama vile 'ngan - o'
(d) Kuandika herufi.isiyofaa kwa mfano 'ongesa' badala ya 'ongeza'
(e) Kuacha herufi katika neno kwa mfano 'aliëkuja' badala ya 'aliyekuja'.
(f) Kuongeza herufi isiyohitajika kama vile 'piya' badala ya 'pia'.
(g) Kuacha alama inayotarajiwa katika herufi karna vile j i.
(h) Kukosa kuandika kistari cha kuendelezea neno a.fikiapo pambizoni au kukiandika mahali pasipofaa.
(i) Kuacha ritifaa au kuiandika mahali pasipofaa, kwa mfano ngombe, ngom' be, n' gombe, ngo'mbe n.k
(j) Kuandika maneno kwa kifupi kama vile k.v., k.m., v.v., u.k.. na kadhalika.
(k) Kuandika tarakimu kwa mfano 27-08-2010.

## ALAMA *ZA* KUSAHIHISHIA

═══ Hupigwa chini ya sehemu anbapo kosa la sarufi limetokea kwa mara ya kwanza tu.

___ Hupigwa chini ya sehemu au neno ambapo kosa la hijai limetokea kwa mara ya kwanza tu.

/ Hutumiwa kuonyesha hoja isipokamilika pambizoni kushoto.

✓ Hutiuniwa kuonvesha kuachwa kwa neno/maneno.
kuonyesha msamiati bora. Alama hii hutiwa juu ya neno lenyewe.

X Hutumiwa kuonyesha msamiati usiofaa. Alama hii hutumiwa juu ya neno lenyewe.

Maelezo mafupi yanahitajika kuhusu tuzo lililotolewa. Kila ukurasa uwe na alama ya chini katikati ili kuthibitisha kuwa mtahini ameupitia ukurasa huo,

## USAHIHISHAJI NA UTUZAJI KWA JUMLA.

Mtahini sharti aisome insha yote akizingatia vipengee muhimu.Vipengee hivi ni maudhui,msamiati,mtindo,sarufi na hijai.

## MAUHDUI

1. Mauhdui ni hoja au mambo yanayozungumziwa,kuelewa au kuhadithiwa kwa mujibu wa mada iliyoteuliwa.
2. Maudhui ndio hasa uti wa mgongo wa insha yoyote ile.
3. Ubunifu wa mtahiniwa hukisiwa kwwa kutathmini uzito wa maudhui yake kulingana na mada teule.

## MSAMIATI

Msamiati ni jumla ya maneno yatumowayo katika lugha husika.Mtahiniwa anatarajiwa kutumia msamiati unaooana na mada teule.Kutegemea ukwasi wa lugha alionao,mtahiniwa anatarajiwa kuikuza mada kwa kuifinyanga lugha kiufundi.Ni muhimu kuelewa kwamba kutokana na maendeleo na ukuaji wa teknologiana mawasiliano,maneno mapya yanaibuka kila uchao.

## MTINDO

Mtindo unahusu mambo yafuatayo.

- Mpangilio wa kazi kiaya.
- Mtiririko na mshikamano wa mawazo kiaya na katika insha nzima.
- Hati nzuri na inayosomeka kwa urahisi.
- Matumizi ya tamathali za usemi ,kwa mfano,methali,misemi,jazanda na kadhalika.
- Kuandika herufi vizuri kwa mfano Jj,Pp,Uu,Ww na kadhalika.
- Sura ya insha.
- Unadhifu wa kazi ya mtahiniwa.

## SARUFI

Sarufi ndio msingi wa lugha. Ufanisi wa mawasiliano hutegemea uwezo wa rntahiniwa wa kitunga ientensi sahihi zenye uwiano wa kisarufi. Mtahini ataonyesha makosa yote ya sarufi yaliyo katika insha anayosahihisha. Makosa ya sarufi huweza kutokea katika:

(i) Matumizi ya alama za uakifishaji
(ii) Kutumia herufi kubwa au ndogo mahali pasipofaa
(iii) Matumizi yasiyofaa ya ngeli na viambishi, viunganishi, nyakati, hali, vihusiano na kadhalika.
(iv) Mpangilio wa maneno katika sentensi.
(v) Mnyambuliko wa vitenzi na majina.
(vi) Kuacha neno linalohitajika au kuongeza neno lisilohitajika katika sentensi.
(vii) Matumizi ya herufi kubwa:
a, mwanzo wa sentensi

## UKADIRIAJI WA UREFU WA INSHA

| | | |
|---|---|---|
| Meneno 9 katika kila msitari | | ukurasa mmoja unusu |
| Meneno 8 katika kila msitari | | ukurasa mmoja na robo tatu. |
| Meneno 7katika kila msitari | | kurasa mbili. |
| Meneno 6katika kila msitari | | kurasa mbili na robo. |
| Meneno 5 katika kila msitari | | kurasa mbili na robo tatu. |
| Meneno 4 katika kila msitari | | kurasa mbili na robo tatu. |
| Meneno 3 katika kila msitari | | kurasa nne nusu. |
| Kufikia maneno | 174 | insha robo. |
| Maneno | 175 – 274 | Insha nusu. |
| Maneno | 275 – 374 | Insha robo tatu. |
| Maneno | 375 na kuendelea | Insha kamili. |

www.eeducationgroup.com

**MTIHANI WA KUTATHIMINI WILAYA YA BONDO - 2015**
**Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)**
102/2
**KISWAHILI**
**Karatasi ya 2**
Julai/Agosti
**MWONGOZO**

**<u>MWONGOZO WA KUSAHIHISHA</u>**

**1.** a) Jutafuata ardhi yenye miti na rutuba — Alama 2

b) - Husababisha mmomonyoko wajuu juu wa ardhi
- Makorongo
- Maporomoko ya ardhi — 3x1=Alama 3


c) - Kutokata miti ovyo
- Kutofyeka nyasina kuacha ardhi tupu
- Kutofuga mifugo wengi
- Kutochoma mioto ovyo
- Kuhifadhi ardhi vizuri — 5× 1=Alama 5

d) Wanafanya kazi nzuri kwa kuwa
i) Wamewahimiza wakulima
- Kupanda zaidi
- Kuhifadhi udongo
- Kutumiani mbolea
- Kunyunyiza dawa makondeni
- Kutumia maarifa malihi katika kupanda mbegu na
ii) Hufundisha wasio wakulima(shule) na kuhimiza kila mmoja kufanya kazi kwa tabasuri na bidii. — 6× ½ =Alama3

e) i) Punguani(Waliopungukiwa akili)
ii) Mkubanyo wa vumbi — 2x1=Alama *2*

2. a) i) Katika kisiwa cha Migingo watu wanaishi pamoja katika vijiji.
ii) Walivianzisha iii kuondoa dhuluma na dhiki
iii) Wanaishi kwa jasho lao
iv) Ushirikiano ndio msingi wa maendeleo/wote wanajitahidi kuleta rnaendeleo
v) Watu wote ni kama ndugu/wanaishi kwa umoja/Hakuna ubaguzi
vi) Wanapenda kazi zao za kilimo/hakuna anayepiga zohali/ni aibu kulaza damu
6x1=Alama 6

b) i) Viongozi na hata wazee wa vijiji hawaingilil sana vijiji hivi
ii) Huhakikisha kuwepo kwa chakula bora
iii) Huhakikisha kwepo maji safi
iv) Huendeleza afya ya watu
v) Hutoa huduma kwa akina mama
vi) Msalaba mwekundu na Mabwana Afya husaidia
vii) Watawala wanatilia kwa watu wazima kuimarisha uvuvi — 7x1=Alama 7




3. a) Tu-Mofimu ya nafsi
Na-mofimu ya wakati
Chez-mzizi/shina

a-kiishio/kimalizio 4x ½ Alama 2

b) i) Ndiwe-kishirikishi kipungufu
ii) aliyecheza-T(halisi) 2x1-Alama 2

c) i) Atumie vielezi/zaidi vinavyofuatana k.rn Mjini Mombasa.
ii) M.f Halii wala kucheka 2x1=Alama 2


d) i) Baadhi ya Nomino huanza na u ambayo hutoweka kwa wingi k.m ukuta-kuta
ii) Mengine huanza na U-Ny k.m Uta-Nyuta
iii) Mengine huanza na U-Nd k.m Ulimi-Ndimi
iv) Mengiine huanza na U-Mb k.m Ubao-Mbao
v) Mengine huanza na U k.m Wembe, wimbo n.k

Zozote 4x1=alama (Maelezo= ½ ,Mfano= ½**)**

e) Unywele wake ulinyolewa wote. 4 x ½ = alama2

f) i) Umilikaji
ii) Kusisitiza 2x1=alama 2

g) i) Levya/lewesha
ii) Lisha 2x1=Alarna 2




8 × ½ =Alama 4

i) i) Mama alisema.
ii) Mama atamlimia.
iii) Atafurahi(Yeye).
iv) Atamlipa vizuri. 4× ½ =Alama2

j) i) Hilo ndilo liliuliwa/sababu ya kuuliwa

ii) Aliua lililolake(bila sababu)
iii) Kwa niaba ya.
iv) Kwa manufaa ya.
v) Lake hilo.
vi) Lake aliyenena — Zozote 2x1=Alama 2

k) Kangumu alisema kuwa✓ masomo yao✓ yangekuwa✓ rahisi rnwaka huo✓

hivyo hawangeumia ✓✓sana. — 6× ½ =Alama 3

I) Alitembea kwa✓ maringo abipokuwa yuko✓/yupo/yumo kule kwao/pale✓

pao/mle mwao(Asichanganye) — 3×1=alama 3

m) i) M'bono-aina ya mti
ii) 'Mbono-mbegu. — 2×1=Alama 2

n) Sentenzi zionyeshe:
i) Amri.

ii) Kauli/Taarifa ujumbe
iii) Swali.
iv) Mshangao au
v) Ombi/rai. — Zozote 2×1=Alama 2

o) i) Kufungia nambari
ii) Kutolea ufafanuzii
iii) Kuonyesha yasiyokuwa ya lazima
k.m Juma(Kijana rnwerevu) amepita rntihani. — Zozote 2x1=Alama 2

p) i) Siimbi silii/Siimbi wala kulia, n.k
ii) Hajaja tena. — *2×1=Alama 2*

q) i) A-WA
ii) Ya-Ya — 2×1=Alama 2

**4.** a) Sheng/mtaani/ya vijana — Alama 1

b) i) Kuehanganyandimi
ii) Lugha sanifu haiturniki
iii) Matumizi ya misirnu
iv) Msamiati maalurnu
v) Silabi chache/sentensi fupi fupi
vi) Mazungumzo ya haraka haraka
vii) Kuna kukatana kali/kalima
viii) Hujikita katika mazingira rnaalumu — Zozote 6×1=Alama 6

c) i) Kuficha siri
ii) Kutomudu lugha zote k.m Kiswahili au Kiingereza
iii) Kujiweka katika kiwango chao(vijana)
iv) Athari ya ukoloni/sabau za kihistoria.

**MTIHANI WA KUTATHIMINI WILAYA YA BONDO - 2015**
**Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)**
102/3
**KISWAHILI**
**Fasihi**
**Karatasi ya 3**
Julai/Agosti- 2015
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. (a) Mashairi huru.hayazingatii arudhi za beti,vina,mishororo,mizani na kibwagizo. (2 × 1 = 2)

   (b) Shairi A – Analalamikia Hadija kwa kumuuwa mumewe kwa kumpa simu.

   Shairi B – Anawalalamikia vijana ambao wanamcheka eti amezeeka na kupitwa na wakati.Wanamramba kisogo. (2 × 2=4).

   (c) Katika shairi A – Hadija alidhani kumuua mumewe angepata suluhisho lakini badala yake amejiletea matatizo zaidi.
   Watu sasawamemsuta kwa kitendo chake na watoto wanamsumbua.

   (d) (i) Amemuua mumewe - mti mkuu au kichwa cha nyumba.
   (ii) Anapata shida za kujitakia. (2 × 2 = 4)

   (e) inkisari - Nendako - Niendako
   - Mwendako - Mnakoenda
   - Bwanako - Bwanako (1 × 2 = 2)

   (f) Mzigo - Uzee / umri
   Siri - Tajriba /Maarifa /Elimu ya maisha.
   Niko nyuma ya wakati - Amebaki nyuma na usasa.

2. (a)
   - Maneno ya Bi.Farashuu.
   - Anamwanbia Biti Kocho.
   - Ni nyumbani kwa Bi.Farashuu - Madongo poromoko.
   - Farashuu alishangaa sababu ya Biti Kocho kuenda kumchukua ili akamsaidie mke wa tajiri wao.
   - Farashuu alifurahi alopotambua kuwa lengo la Biti Kocho ni kumsaidia kulipiza kisasi.
   - Kwa uchungu mwingi alieleza maovu ya Maaksudi na urafiki wake ndipo akasema manena haya.

   (Hoja 4 × 1= alama 4)

   (b)
   - Kazija alifanya njama ya kumfumanisha Mussa na babake.
   - Alimpa Mussa miadi ya kufika saa tatu na Maaksudi akamwambia afike saa sita.
   - Maaksudi alipokutana na Mussa alimpiga nusura amwue.
   - Mussa alilazimika kuchopeka vidole vyake kwenye macho ya babake na akafaulu kutoroka.
   - Alipoachiliwa hakuonekana tena nyumbani kwao na hata kwa Kazija – alitengana na babake.
   - Alizomewana Kazija na akalazimika kurudi nyumbani usiku wa manane kwa miguu.
   - Haya yote yalipangwa na Farashuu ili kukamilisha kisasi cha mateso aliyofanyiwa Mwanasururu na Maksudi.
   - Usiku huo huo Maimuna alitoroka kwao na kwenda kumtafutia mamake mkunga - anakaidi amri na kutoka nje.
   - Kisha baada ya kurudi nyumbani usiku hou,alitoroka kwao ili kutafuta uhuru baada ya kuonja uhuru wa usiku moja.
   - Maksuudi anaporudi anamlaumu Tamima na kumpiga sana kasha kumtaliki.
   - Hatimaye Kazija anamfedhehesha katika uwanja wa uhuru.

- Baadaye anatumikia kifungu cha miaka miwili baada ya kupatikana na makosa ya jinai.

(c)
- Mwenye bidii.
- Mwenye kisasi.
- Katili.
- Mnafiki.
- Mkarimu
- Mshirikina.
- Msiri.
- Msamehevu.
- Mpole /Mtulivu.
- Mwenye majuto.
- Mwenye huruma.

3. Maana ya methali :Anayekuwa na tama ya kupata kitu ,anapokipata kinaweza kumdhulumu.

(i) Maimuna
- alikiwa na tama ya kupata uhuru.
- Aliingizwa katika maisha ya ukahaba na ulevi.
- Anasingiziwa wizi kwa Mama Jeni na kufukuzwa.
- Anapigana na kijakazi kule kwa Bit Sururu.
- Alidhoofika kiafya.

(ii) Mussa
- alikuwa na tama ya ukware na Kazija.
- Alifumanishwa na babake nusura auawe.
- Alilazimika kutoroka na kutenganishwa na jamaa yake.

(iii) Maksuudi
- Alikuwa na tama ya kupata mali.
- Alikuwa na tama ya kimapenzi na kazija.
- Alikuwa na tama ya uongozi.
- Alimnyanganya Mwanasururu mali yake na kumtaliki. Hili linamfanyya Bi.Farashuu kulipiza kisasi dhidi yake.
- Alishikwa na kufungwa kifungu cha miaka miwili gerezani.
- Anafumanishwa na mwanawe Mussa kwa Kazija.
- Kazija anamfedhehesha katika uwanja wa uhuru.

(iv) Bi.Farashuu
: Alikuwa na tama ya kulipiza kisasi ya Bw.Maksuudi.
- Alisaidiana na Biti Kocho kumtorosha Maimuna.
- Hatimaye Maimuna aliyemtorosha ndiye anayekuwa mke wa mjukuu wake.
- Hatimaye anajutia kifo cha Mksuudi.

(v) Zanga
- Alikuwa na tama ya kupata mali.
- Alikuwa na tama ya uongozi.
- Anashiriki katika kesi za ufisadi na kushikwa na kutumikia kifungu cha miaka miwili gerezani.
- Anafedheheshwa na Kazija katika uwanja wa uhuru.

6. (a) Haya ni mawazo ya Fikirini akiwa kule nyumbani kwa Fiona na Bob.
- Alikutana na mwanamke chuoni baada ya kuachiwa kimaksudi na basi
- Fiona anamhadaa kuwa anampeleka chuoni.Naye Fikirini kwa wepesi wake wa kushawishika anamfuata.
- Anajipata amefungiwa nyumbani,ameporwa kidogo alochokuwa nacho na sasa anatishiwa kuuwawa.
- Ni katika hali hii anapowaza yaliyomo dondooni.

(Hoja 4 × 1 = 4)

(b) (i) Takriri: Siku ya Siku,Siku,Siku,kufa na kifo.
Mbinu hii inatumika kubainisha maudhui mazito kwa maana ya mkato.Pia hufanya masimulizi kuvutia. (2 × 3 = 6)

(c)
- Msomi
- Mvumilivu

- Ana msimamo thabiti.
- Ni mzalendo.
- Ana utu.
- Mwoga.
- Anashawishika haraka.

(Zozote 5 × 2 = 10)

7.

Swa1i: Linganisha na ulinganue maudhui ya ushirikina katika hadithi ya *Gilasi ya Mwisho Makaburini* na hadithi ya *Kikaza* ——— *(alama* 20)

Ushirikina ni imani fulani ya jamii au ya wanajamii kuhusiana na jambo, hali au matukio fulani. Maudhui ya ushirikina yametawala hadithi nzima ya *Gilasi ya Mwisho Makaburini.* Msoi aliota ndoto za kishirikina na kuziamini. Aliota ndoto zilizomwambia kwamba mahala walipozoea kwenda yeye na marafiki zake kupitisha wikendi, palikuwa mahala pa wafu. Msoi aliamini sana ushirikina huu kiasi cha kukataa kwenda katika Baa ya Makaburini. Hali hii inaashiria ushirikina ulivyokita mizizi katika akili ya Msoi.

Msoi anapojikwaa miangoni na bakuli lake la maua likavunjika vipande vipande, hali hii iliibua imani fulani ya kishirikina. Kwake hiyo ilikuwa ishara mbaya iliyomtahadharisha dhidi ya mabaya ambayo yangetokea baadaye.

Matukio mabaya yakifuatana kulingana na Msoi ni onyo ya kitu kibaya ambacho kitatokea baadaye. Bakuli la Msoi lilipovunjika kisha mguu wake wa kushoto kukosea mizani, akapepesuka na kutaka kuanguka, Msoi aliamini kuwa matukio haya yanamtahadharisha kuhusu tukio mbaya. Huu ni ushirikina.

Semkwa aliyeyafuatilia matukio mabaya yakimfanyikia Msoi, alisema kuwa kweli itikadi na ushirikina vilimdhibiti Msoi. Hapa ni baada ya Msoi kujibana kidole kidogo akatoa usiyahi alipokuwa akifunga miango wa gari. Njiani, Msoi na marafiki zake walipokuwa wakielekea kwenye Baa ya Makaburini hali ya anga ilibadilika ghafla, kukawa na mngurumo na radi iliyopasua mbingu. Hali kama hii huashiria kunyesha kwa mvua. Hata hivyo, mvua haikunyesha. Msimulizi anasema kuwa hiyo ilikuwa ishara mbaya kwa Msoi. Hii ni imani ya kishirikina.

Msoi alipobadilisha mahali pake alipozoea kukaa kwenye Baa ya Makaburini, kisha anamchokoza kutokana na hali yake ya kuamini katika ushirikina.
Anasema kuwa siku hiyo Msoi alibadilisha makao ili apate mandhari mazuri ya mava. Hii ni imani ya kishirikina.
Josefina aliamini katika ushirikina. Anasema kuwa Msoi akishikj kama Ziraili mpaka aitoe roho ya kiumbe. Imani za kishirikina zinaj hapa ambapo Josefina anasema kuhusu Ziraili. Inaaminika Ziraili ni malaika wa mauti ambaye huleta vifo katika jamii.

Kundi la vizuu lilipoonekana kwenye maya, watu wote walipiga wakikimbilia usalama wao. Watu hawa waliamini katika ushirikina wakakimbilia usalama wao wakipiga ukwenzi.

Kwa upande mwingine, maudhui ya ushirikina yamejitokeza pia katika hadithi ya *Kikaza.* Wanakijiji katika hadithi ya *Kikaza* wanaamini mam ushirikina. Mvua ilipoacha kunyesha walikuwa katika makundi wakijadili kuhusu hali ya mvua kutonyesha.

Wanakijiji walienda kwa Mzee Babu kuteguliwa kitendawili cha r kutonyesha. Mzee Babu aliwaambia wawaulize washona kikaza. waliamini kuwa mvua ilikosa kunyesha kwa sababu ya kikaza.

Mzee Babu aliamini katika mambo ya ushirikina. Aliwaambia wana kila mara kuwa si kila

panapo mawingu meusi na mazito mvua hunye Aliwaeleza kuwa mengine huwa meusi kutokana na mchafuko wa mazin na hata ingenyesha maji yake huwa si mazuri.
Mzee Babu aliamini kuwa kila aingiaye kwake lazima apate chakula au hata kinywaji ili azungumze naye. Aliamini kuwa angepata baraka kutokana ukarimu wa kuwalisha wageni wake. Hizi ni imani za kishirikina.

Wanakijiji waliamini kuwa kita wanapovuna, sehemu ya mavuno ya mimea lazima wapeleke kwa Mzee Babu ili mashamba yao yaweze kubarikiwa. Hizi ni imani za kishirikina.

Ni imani ya kishirikina kuwa kikaza, yaani suruali ya ndani ya kiongozi wa kiume, lazima ipimwe na mwanamume na ishonwe na wanawake kikaza cha kiongozi wa kike lazima kipimwe na mwanamke na kushonwa na wanaume.

Ni imani ya kishirikina kwa Mzee Babu kuamini kuwa kuwajibu wanal kwa mafumbo ni busara. Mzee Babu anatoa majibu yake kwa mafumbo. Anawaeleza wanakijiji wawaulize washona kikaza kisha anawaamia hadithi ya kobe na gamba lake.

8. (a) (i) Sifa za hurafa.
- Ni hadithi.
- Wahusika aghalabu huwa wanyama.
- Wahusika hupewa sifa na matendo ya binadamu.
- Huwa na mafumbo.

(Zozote 2 × 1=2)

(ii) Sifa za mighani.
- Ni hadithi za mashujaa.
- Ni hadithi za kihistoria.
- Wahusika huwa mashujaa.
- Hupigania haki za wanyonge.

(Zozote 2 × 1 = 2)

(iii) Sifa za Maviga.
- Hujumuisha vitendo maalum k.v kuimba,kuruka na kucheza ngoma.
- Huhusisha maombi.
- Aghalabu wahusika hutoa sadaka.
- Wahusika huweka ahadi(kiapo)
- Kuna matumizi ya vifaa,mavazi na mapambo maalum.

(Zozote 2 × 1=2)

(b) Umuhimu wa ngomezi.
- Hutoa taarifa kwa njia nyepesi na kuwafahamisha wanajamii kuhusu matukio fulani k.v sherehe,mkutano.
- Hutumika kutahadharisha watu.
- Hutumika kutoa matangazo rasmi.
- Ni njia ya kudumisha utamaduni.
- Ni njia ya kidhihirisha ufundi wa jamii.

(6× 1 =6)

(c) Sifa za Mafumbo.
- Ni semi ambazo hufumba macho.
- Huhitaji mtu kuwaza ili aweze kubaini fumbo lenyewe.
- Baadhi ya mafumbo hufananisha kitu kilichotajwa katika fumbo na mazingira halisi.
- Baadhi ya mafumbo huwa marefu na mengine huwa mafupi.
- Mafumbo huhitaji mantiki ili kuyatambua.

(4 × 1 = 4)

(d) Tofauti kati ya malumbano ya utani na mawaidha.

| Mawaidha | Malumbano |
|---|---|
| (i) Hutolewa na watu maalum katika jamii | (i) Wahusika hukubaliana kufanyiana utani |
| (ii) Hutolewa na wakubwa kwa wadogo | (ii) Hutokea kwa njia ya malumbano au kujibizana. |
| (iii) Mawaidha hutumia lugha ya kipekee kuahdiri na kuvuta nadhari. | (iii) Mtani hutumia lugha ya ucheshi na upigaji chuku. |

Zozote 2× 2 = 4